

SHUGHULI ZA UWEKEZAJI WILAYA YA MUHEZA

Maeneo ya uwekezaji

Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imeainisha aina na maeneo ya uwekezaji kuwa ni Uzalishaji na usindikaji wa matunda, Uzalishaji na usindikaji wa mazao ya viungo, Uzalishaji wa mpira, Utalii, Hoteli na Uvuvi.

1. Uwekezaji katika kilimo

Kilimo cha matunda hususani machungwa na matunda mengine yanayostawi zaidi katika Wilaya ya Muheza kama maembe, mananasi, mafenesi n.k. Maeneo mawili yameainishwa kwa ajili ya uwekezaji kilimo ambayo ni:

❖ **Shamba la Sigi Miembeni;**

Shamba lina ukubwa wa Hekta 3,036.36 na limepimwa, eneo la ardhi lililotengwa kwa ajili ya uwekezaji ni Hekta 892.1 na utaratibu wa uwekezaji utakaotumika ni ubia au Kuuza.

❖ **Kilimo cha Mazao ya viungo**

Viungo vinavyostawi katika Wilaya ya Muheza ni Iliki, Mdalasini, Karafuu, Pilipili manga na Kakao. Uzalishaji na uuzaji wa viungo ni wa chini ingawa kuna maeneo mazuri ya uzalishaji. Kuna ukuaji mkubwa wa mahitaji ya mazao ya viungo duniani ikiwa uzalishaji utakuwa na ubora hasa kilimo kisichotumia mbolea za viwandani. Soko la nje ni kama Afrika ya kati, Asia, Ulaya, Afrika na Amerika. Soko la ndani linajumuisha Zanzibar na Tanzania Bara

❖ **Zao la Mpira**

Eneo lililotengwa ni Kihuhwi shamba la Bwembwera lenye ukubwa wa hekta 2,300. Uzalishaji wa mpira kibiashara bado haujaendelezwa hapa Tanzania kiujumla, Uzalishaji wa Mpira katika Tarafa ya Bwembwera ni mkubwa na kama utaendelezwa bidhaa nyingi zinazotokana na mpira zitazalishwa.

1. Uwekezaji katika sekta ya Viwanda

Kupitia makongamano ya Uwekezaji ambapo fursa za uwekezaji zilitangazwa na Wawekezaji walionesha nia ya kuwekeza katika Halmashauri, hadi sasa hatua zilizofanyika ni kuenga eneo lenye ukubwa wa ekari 10 kwa ajili ya uwekezaji wa kiwanda cha kusindika mhogo kwa mwekezaji Community Money Transfer Limited (CMTL). Mwekezaji anaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha (Capital) kutoka UN na kufanya utafiti juu ya takwimu za uzalishaji wa machungwa ambapo Sampuli za machungwa zimechukuliwa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara ili kubaini ubora wake ambapo imeonekana kuwa machungwa ya Muheza yanafaa, aidha mazungumzo juu ya uwekezaji huo yanaendelea kufanyika baina ya MUVI kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na mwekezaji (Teampro - Muungano wa Makampuni ya Uholanzi).

2. Utalii wa Ikolojia na wa Kiutamaduni

Yapo maeneo kadhaa ambayo ni vivutio vya aina hii ya Utalii. Maeneo hayo ni pamoja na hifadhi ya asili ya Amani ambapo wanapatikana viumbe adimu ulimwenguni, vivutio

vingine ni ufugaji wa vipepeo eneo la Amani, Maporomoko ya maji ya Mto Zigi, Ua la St Paulia, Mlima wa Mlinga, kanisa la kwanza la Angalican katika Tanzania- Utalii unajumuisha maeneo mazuri ya fukwe yaliyopo katika kata ya Kigombe. Uwekezaji katika sekta hii ni muhimu ili kukuza sekta ya utalii. Hii inajumuisha ujenzi wa hoteli za kitalii na ufugaji wa vipepeo.

3. Uwekezaji katika sekta ya uvuvi

Katika Wilaya ya Muheza shughuli za uvuvi zinafanyika katika bahari ya Hindi eneo la Kigombe. Uzalishaji wa samaki katika eneo hili ni mkubwa na unahitaji kuendelezwa. Uvuvi katika Wilaya ya Muheza unahusisha uvunaji wa samaki katika mabwawa, hivi sasa yapo mabwawa 84 yanayotumika kati ya mabwawa 128 yaliyopo. Hata hivyo ufugaji unaofanyika katika mabwawa kwa sasa ni kwa ajili ya matumizi ya chakula kwa mfugaji husika (Domestic use). Endapo mabwawa haya yataendelezwa uzalishaji wa samaki utaongezeka kwa kiasi kikubwa. Vichocheo katika uwekezaji huu ni kuwepo kwa miundombinu ya barabara (Barabara ya Tanga- Kigombe- Pangani), aina za samaki zilizopo na bwawa jipya la Misozwe ambayo yana nafasi kubwa ya uendelezaji.

4. Uwekezaji katika Sekta ya Huduma

Wilaya inayo maeneo ya yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa huduma za jamii ikiwemo Viwanja kwa ajili ya Ujenzi wa Shule za Sekondari na chuo kikuu. Eneo lipo lenye ukubwa wa Ha 5.3 na limefanyiwa upimaji wa awali (Dermacation) na katika shamba la chartur lipo eneo la ujenzi wa chuo kikuu. Eneo lenye ukubwa wa Ha. 2 limefanyiwa upimaji wa awali (Dermacation) lipo katika Kata ya Kwemkabala na Ha. 1.5 lipo katika Kata ya Magila, Kijiji cha Mkwakwa Mafleta.

5. Eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya

Eneo lenye ukubwa wa Ha. 1 lipo katika Kata ya Kilulu na limefanyiwa upimaji wa awali (Dermacation).

Maeneo kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba za makazi (Housing Estate) yapo mawili; eneo la Chartul lenye ukubwa wa Ha 1.7 limeshapimwa na upimaji wa awali (Dermacation) umefanyika, na Ha 1.4 zimetengwa katika eneo la Kwemkabala